TANGAZO LA SERIKALI NA. 202 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1)(b))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA KUZUIA NA KUDHIBITI SUMUKUVU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA YA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 411 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Kuzuia na Kudhibiti Sumukuvu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ya Mwaka 2025, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya Kuzuia na Kudhibiti Sumukuvu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama “Sheria Ndogo kuu”.

Marekebisho ya kanuni ya 16

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 16 kwa-

(a) kuongeza maneno “bila kuwa na sababu ya msingi” mwanzoni mwa aya za (a), (b) na (c);
(b) kufuta neno “hataanika” lililopo mwanzoni mwa aya ya (d) na badala yake kuweka neno “ataanika”; na
(c) kwa kubadili mpangilio wa aya (k) kuwa maneno ya kufungia.

Kuongeza kanuni mpya ya 16A

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kanuni ya 17 kanuni mpya ifuatayo:

“Adhabu

17. Mtu atakayepatikana na hatia chini ya Sheria Ndogo hii atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote kwa pamoja.”.

Kufuta na kuiandika upya kanuni ya 17

4. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 17 na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"Kufifilisha kosa

18. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kujaza fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili na kulipa ushuru anaodaiwa.".

Dodoma,
10 Januari, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi – OR-TAMISEMI*